

# Juhudi za Petra Diamonds kusafisha historia yake mbaya nchini Tanzania

*Changamoto katika kupata fidia na kurejesha mahusiano na jamii baada ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika mgodi wa almasi wa Williamson*

MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

IPIS

IPISRESEARCH.BE

# MUKTASARI

## Usuli

Ripoti hii inatathmini juhudi za Petra Diamonds za kurejesha mahusiano kwa jamii na alama njema baada ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika mgodi wake wa almasi wa Williamson nchini Tanzania. Ripoti kuhusu ukiukwaji zilienea bila kufanyiwa kazi kuanzia takriban 2011. Walijumuisha madai ya kupigwa, mateso, kuwekwa kizuizini kinyume na sheria, ufyatuaji holela wa risasi, unyanyasaji wa kijinsia na mauaji ya wenyeji wanaoingia katika eneo kubwa la biashara la Williamson Diamonds kutafuta almasi, kuchunga mifugo au kutafuta kuni.

Mwaka 2020, kampuni ya sheria ya Uingereza Leigh Day, ilifungua kesi katika Mahakama Kuu ya Uingereza kwa niaba ya wahanga na familia zao dhidi ya Petra kama mmiliki mkuu wa Kampuni ya Williamson Diamonds. Kesi hiyo ilisababisha uongozi wa juu wa Petra kuanza kujichunguza juu ya tuhuma hizo, ambazo zilithibitisha upotevu wa maisha, kuumia na kutendewa vibaya kwa wavamizi kulikofanywa na walinzi binafsi wa mgodi huo na polisi waliokuwa wanafanya kazi kwenye eneo la Williamson Diamonds.

Mnamo Mei 2021, Petra ilikubali kufanya makubaliano ya kumaliza mgogoro kati yake na walalamikaji 96 wa Kitanzania, ikiahidi kitita kizito chenye thamani ya takriban € milioni 5. Kitita hiki kilimaanisha fidia kwa wahanga, miradi ya maendeleo ya jamii na kuanzishwa kwa baraza huru la malalamiko ili kuzuia madhara yasijitokeze zaidi. Tangu wakati huo, Petra imeiachia Kampuni ya Williamson Diamonds hisa zake nyingi - zilizopatikana tangu 2009 - ingawa bado ina hisa kubwa.

## Kiini cha ripoti hii

Kati ya Julai 2022 na Oktoba 2023, Shirika la IPIS lilifanya tathmini ya jinsi makubaliano ya kisheria ya 2021 yanavyotafsiriwa na athari walizopata wakazi wa vijiji vilivyo karibu na mgodi wa Williamson. Lilifanya utafiti wa kina wa uwandani, ikiwa ni pamoja na mahojiano zaidi ya 120 na wakazi wa eneo hilo, asasi za kiraia na serikali za mitaa, pamoja na kuwashirikisha wadau muhimu, ikiwa ni pamoja na Petra. Utafiti huu wa msingi ulifuatiwa na uchambuzi wa kina wa ripoti ya shirika, ripoti za vyombo vya habari na uchunguzi uliofanywa na asasi za kiraia na wadau wengine.

Katika kutaka kuelewa mahitaji ya leo, uchambuzi wa IPIS kwanza ulichunguza kile kilichoenda mrama kipindi cha nyuma. Kimahususi, ilihoji namna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu haukushughulikiwa kwa muda mrefu. Petra inasema, yenyewe kwa sehemu inalaumu miundo ya utoaji ripoti: Uongozi wa juu wa Williamson Diamonds na Petra ulikuwa unajua matukio na vifo vingi lakini hawakuijulisha bodi ya Petra. Sababu ya pili ilikuwa ni dhana (iliyosababishwa na Petra katika kujinadi kwake yenyewe) kwamba Petra ni mchimbaji wa almasi mwadilifu na anayesimamia vema masuala ya Mazingira, Jamii na Utawala (ESG). Hii iliwarahisishia wale waliokuwa wanajua tuhuma kusema tu kwamba wanapaswa kufukuzwa kwa kuwa hawajathibitisha hilo la msimamo wa Petra. Kwa hiyo, walionekana tu 'wana dhamira kubwa' mara tu walipoona sifa hiyo njema inakaribia kupotea – na ikaonekana wazi hivyo. Tatu, sauti za ukosoaji zinaendelea kutosikika kutokana na ripoti zinazoendelea za kuwafanya wahanga wawe ndio wenye hatia na kuwasafisha wahusika katika muktadha wa Tanzania. Mwisho, utafiti wa IPIS unaonesha kuwa mgodi ulikosa miundo thabiti ya kuishirikisha jamii na namna ya kushughulikia malalamiko. Udhaifu huu ulikuwa umeziweka mbali kabisa Petra na Williamson Diamonds na muktadha wa wazawa ambako walikuwa wakifanyia kazi, na kusababisha pande zote mbili kuonekana kuwa na uelewa mdogo juu ya motisha, wasiwasi, malalamiko au matarajio ya kila mmoja.

Kumaliza mgogoro na Petra kunaweza kuonekana kama kushughulikia mambo yaliyoshindikana zamani kwa njia kuu tatu: kwa kutafuta kuboresha mahusiano na jamii, kupunguza madhara yanayoweza kutokea zaidi, na kuboresha upatikanaji wa fidia. Kuchambua jinsi juhudi kupitia maeneo haya matatu ya mkazo zinavyotafsiriwa na kuathiri jamii zinazoishi karibu na mgodi, kumewezesha IPIS **kujibu maswali matatu maalum ya utafiti**, kama ilivyoelezwa katika ripoti hii:

1. Je, Petra na Williamson Diamonds watafanikiwa kujenga mahusiano mazuri zaidi na jamii zinazoishi karibu yao, na kuondokana na kutoaminiana, kuchanganyikiwa, sonona na chuki ambazo zimejengeka ndani ya jamii hizi kwa zaidi ya muongo mmoja?

2. Je, wataweza kuzuia madhara zaidi yasitokee, ikiwa ni pamoja na kulinda ardhi na rasilimali walizopewa na Serikali huku wakiheshimu haki za binadamu?

3. Je, watasimamia kazi ngumu ya kutoa kwa usawa na haki fidia kwa wahanga wote wa ukiukwaji wa haki za binadamu na malalamiko mengine?

### Kuboresha mahusiano na jamii

Mbali na mpango mpya wa kuwahusisha wadau, juhudi za Petra za kuboresha mahusiano na jamii ni pamoja na 'miradi kadhaa ya kurejesha haki'. Mipango hii ya kukuza maendeleo endelevu katika vijiji vya karibu bado iko katika hatua ya awali. Inahusisha kampeni ya kupambana na unyanyasaji wa kijinsia, ukataji kuni unaoratibiwa kwenye eneo la mgodi, mpango wa maendeleo ya kilimo biashara, na msaada kwa wachimbaji wadogo (ASM). Mipango hii ina uwezo mkubwa wa kuboresha mahusiano yatakayoshughulikia kwa kiwango mahitaji halisi ya maisha ya wakazi. Hata hivyo, ina hatari ya kuamsha hisia kutokana na ahadi za zamani ambazo hazikutekelezwa kama matarajio na mawasiliano kwenye miradi hii hayatasimamiwa vema. Kwa mfano, habari kwamba mgodi unaweza kusitisha mipango iliyotangazwa ya kusaidia wachimbaji wadogo inaweza shubiri kwa wanajamii. Wanategemea sana mfumo huu wa maisha na wameona kwa miaka 15 iliyopita mipango kama hiyo mara nyingi ikiachwa kutekelezwa.

### Kupunguza madhara yanayoweza kutokea zaidi

Hatua kadhaa pia zilichukuliwa ili kupunguza uwezekano wa kusababisha au kuchangia madhara mapya. Matukio ya kuvamiwa na wavamizi ni kiini cha madhara mengi na makubwa yanayowakabili wenyeji waishio karibu na mgodi. Ili kupunguza matukio kama hayo, Petra na Williamson Diamonds waliboresha mipaka ya eneo la mgodi, wakapitisha kanuni mpya za kusimamia usalama wa mgodi, na kugawa nafasi ya mkandarasi binafsi wa ulinzi aliyelalamikiwa sana, Zenith Security kwa GardaWorld mnamo Machi 2021.

Kisichoshangaza ni kwamba, uvamizi wa wenyeji kwenye eneo hili haujaisha. Wafugaji wanaofuatilia, kuongoza au kutafuta mifugo yao kwenye eneo hili ambalo halina uzio mara nyingi wamekuwa wanalalamika kwamba wananyang'anywa mifugo, na kulipishwa faini kubwa kabla ya kurejeshewa hiyo mifugo. Aidha, uchimbaji mdogo wa almasi kwenye eneo la uwekezaji la Williamson unaendelea kukua, na kuchukuliwa kwa ujumla na jamii kama mkakati halali wa maisha unaosaidia kupata madai yasiyotimizwa kwenye eneo lenye utajiri wa almasi na manufaa mengine.

Wakati watoa taarifa wengi wa IPIS wanakubali kwamba vurugu katika mgodi huo zimepungua, zimekuwa si za kibaguzi sana na hazisikiki sana, IPIS bado imepokea ripoti mbalimbali za vipigo. Zote hizi zinaeleza kwamba walinzi wanawapiga wavamizi kwa fimbo kwenye vifundo, mikono na miguu, kabla ya kuwaachilia au kuwakabidhi kwa polisi. Ripoti za mashambulizi ya risasi zimekuwa nadra sana tangu kuondoka kwa Kampuni ya Ulinzi ya Zenith.

Mbali na hili, IPIS imepata **ushuhuda unaoogofya** kutoka kwa mchimbaji mdogo wa madini ambaye alipata majeraha makubwa ya risasi mnamo Januari 2022. Anadai kuwa alipata majeraha haya mikononi mwa walinzi wa Kampuni binafsi ya Williamson Diamonds. Alipoulizwa na IPIS kutoa maoni wakati wa maandalizi ya ripoti hii, Kampuni ya GardaWorld, kwa upande wake, inadai kuwa ina taarifa kwamba mtu huyu alikuwa mhanga kwenye kulinda mgodi jirani wa almasi wa El-Hilal. Mbaya kwa mgodi wa Williamson, kijana huyu aliwasilisha malalamiko kwenye baraza huru la malalamiko mnamo Mei 2022, lakini hadi tunachapisha ripoti hii - yaani zaidi ya miezi 16 baadaye - bado hakuwa amepokea mrejesho. Bila kujali ukweli uliopo kwenye kesi hii, kutojibu tuhuma za unyanyasaji unaoendelea kunaibua wasiwasi mkubwa juu ya uwezo wa Williamson Diamonds kuzuia unyanyasaji zaidi - uwe wa mfumo mzima au wa mtu mmoja mmoja- kwa siku zijazo. Kutokana na historia ndefu ya unyanyasaji katika mgodi wa Williamson, kusita kujibu tuhuma kubwa kama hizo kunaibua wasiwasi mkubwa juu ya vipaumbele, utayari na utoshelevu wa njia mpya ya mgodi kushughulikia malalamiko na kulinda dhamira safi ya Petra. Kuanzishwa kwa baraza huru la malalamiko ni jambo la kupongezwa, lakini hakuyaondolei makampuni majukumu yao ya kuchukua hatua kulinda haki za binadamu kupitia maamuzi na miundo ya kuzuia madhara, kama ilivyoelezwa katika Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu.

Ikiwa bado inapambana kupunguza madhara na kurejesha uaminifu, Williamson Diamonds ilikuwa chanzo cha uharibifu zaidi kwa ngazi ya mtu binafsi na ya jamii Novemba 2022, wakati bwawa la kuhifadhi maji **yakuchenjulia makinikia** lilipopasuka na kusababisha matope kuzagaa majumbani, mashambani na kuingilia mifumo ya usambazaji wa maji vijiji kadhaa. Wataalamu wanasema kwamba ajali hii mbaya ingeweza kuepushwa kama viwango vya ufuatiliaji sahihi vingefuatwa. Miezi iliyofuata baada ya bwawa kupasuka, wenyeji wengi wamejitahidi kukidhi mahitaji yao ya msingi na kuendelea na maisha yao

kupitia kilimo na uchimbaji mdogo. Pamoja na kutokuwa na uhakika na kuchanganyikiwa juu ya jinsi athari mbaya zingeepushwa, tukio hili liliamsha hisia za kutouaminika kwa mgodi.

### Kupata fidia kwa ajili ya madhara ya zamani na mapya

Petra na Williamson Diamonds zinajaribu kukomesha ukosefu wa uwajibikaji na fidia kwa ajili ya madhara yanayosababishwa na au kuhusishwa na shughuli na mipango yao ya usalama. Wameanzisha baraza la malalamiko ya jamii (CGM) kwenye masuala ya kila siku ya uendeshaji, baraza huru la malalamiko (IGM) kwa wahanga wa ukiukwaji wa haki za binadamu, na utaratibu wa dharura kwa wale walioathirika na kupasuka kwa bwawa la kuhifadhi maji ya kuchenjulia makinikia. **Taratibu hizi tofauti za kushughulikia migogoro** zinawaongezea sana wenyeji imani ya kupata fidia na hivyo kuongeza upatanisho na kunusuru uhusiano kati ya mgodi na jamii za karibu. Hata hivyo, utafiti wa ripoti hii unaonesha kwamba taratibu zote hizi tatu zinafanana kwenye mambo manne, ambayo lazima yashughulikiwe ili kufanikisha hili kisawasawa, ambayo ni kushindwa kubashiri vema, uwazi, usawa na majadiliano.

Kutokana na kiwango na athari kubwa za ukiukwaji wa nyuma wa haki za binadamu, utekelezaji wa **baraza huru la malalamiko** lililo chini ya la Petra ndo kiini cha utafiti wa ripoti hii. Kuna nyaraka chache kwa ajili ya umma juu ya muundo na utendaji wake, ambazo zimesababisha mkanganyiko usio wa lazima baina ya walalamikaji. IPIS imechora picha ya utaratibu huu kwa kutumia utafiti wake na taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali juu ya utendaji kazi wa baraza hili. Hii inaonesha kwamba muundo ni thabiti, na kuna juhudi kubwa za kutafakari vigezo vingi bora vya kiutendaji kupitia taratibu za malalamiko kwa ngazi ya kampuni kama ilivyoainishwa katika Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu. Njia hii ya kutumia baraza huru bila kuhusisha mgodi kwa kutumia wataalam wa Kitanzania inachangia kwa kiasi kikubwa kufikika na uhalali wake. Kufikia Novemba 2022, watu 5,575 walikuwa wamepeleka malalamiko kwenye baraza - ushahidi wa kufikia juhudi za kukuza uelewa wa mgodi wa Williamson kuhusu uwepo wa baraza hilo, pamoja na kumbukumbu juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu katika mgodi huo.

Licha ya nyenzo hii ya uhakika, utafiti wa IPIS hata hivyo umegundua kuwa baada ya usajili, mchakato huo **haukuwa wa kutabirika na wazi** kwa idadi kubwa ya walalamikaji 360 waliochaguliwa kama sehemu ya awamu ya majaribio ya IGM. Kutopatikana kwa habari kunawachanganya walalamikaji kuhusu upeo - ikiwa ni pamoja na muda - wa IGM, na pia kujenga kutokuwa na uhakika juu ya kile kinachotarajiwa kutoka kwao, ushahidi unaohitajika, jinsi ya kupata ushahidi huo, matokeo gani wanaweza kutarajia, na lini wanaweza hata kupata hayo matokeo. Wale wanaoombwa kuanza na sehemu muhimu ya mchakato hawapewi taarifa ya juu ya kuandaa ratiba yao au kujiandaa vya kutosha. Hii ni chanzo cha mafadhaiko makubwa na wasiwasi, ambayo inaimarishwa zaidi na ukosefu wa uwazi juu ya hali ya madai na maendeleo ya jumla ya IGM. Tangu usajili, walalamikaji wengi hawajasikia chochote kuhusu kesi yao, au IGM kwa ujumla, kwa nini (wakati wa kuchapishwa) itakuwa hadi miaka miwili.

Miongozo mingine miwili bora ya kuzingatia ambayo inaonekana kupuuzwa kutekelezwa na IGM ni **usawa na majadiliano**. Walalamikaji wengi waliohusishwa kwenye utafiti na IPIS wanaona mchakato huo ni wa kipingamizi. Hii inahusisha hasa wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia kwani inaonekana kuwa hakuna hatua za kutosha zimechukuliwa kuzuia au kupambana na sonona mpya, unyanyapaa na changamoto za ushahidi. Kinacholeta wasiwasi tena ni kwamba - kinyume na kile Petra amedhamiria - hakuna hata mmoja wa walalamikaji waliohojiwa na IPIS anayeonesha kuwa alipata “msaada wa bure na huru wa kisheria” wakati wa maandalizi au kushughulikia malalamiko. Ni walalamikajii wachache tu ambao walikuwa wamefikia hatua ya mwisho ya uamuzi walisema kuwa walikuwa wametambulishwa kwa mwanasheria kwakuwa jopo la IGM lilikuwa limewajulisha juu ya uamuzi wao. Ukosefu huu wa msaada wa kisheria, na hisia iliyopo ya mchakato wa kupelendela upande mmoja na usio jumuishi, umesababisha walalamikaji wengi kuhoji uhuru wa mpango huu. Hisia hii inakolezwa na ripoti za makosa na changamoto katika utaratibu wa IGM, ambao walalamikaji wanaachiwa muda wa kutafakari na kulifanyia kazi wenyewe.

Mfumo huu ambao ulijaribiwa katika awamu ya majaribio haukulingana na kile kilichoahidiwa kutokana na vipengele kadhaa muhimu, wakati ni wazi kabisa walalamikaji wanapata shuruba. Ripoti ya kwanza ya wachunguzi huru wa IGM, iliyochapishwa muda mfupi kabla ya kutolewa kwa ripoti ya sasa mnamo Oktoba 2023, inaonyesha wanajua mapungufu kadhaa ya hapo juu. Inathibitisha kuwa IGM ilizinduliwa bila maandalizi ya kutosha ya kuendana na ukubwa wa kazi iliyopo, na sasa **inapachikwa viraka kadri inavyoendelea** zaidi ya awamu ya majaribio. Juhudi kadhaa zimeripotiwa

kufanyika katika kushughulikia kasoro kubwa, kama vile lugha ya matusi na ya kufokeana inayotumiwa na wafanyakazi wa IGM. Inasemekana pia mabadiliko mengine, kama vile ushirikishaji na mawasiliano bora kwa walalamikaji na jamii, yanaendelea kufanyiwa kazi. Bila shaka, ukweli na uwazi ambao ripoti ya IPIS yenyewe itatoa kwa walalamikaji unaweza kuchangia katika kujifunza zaidi na itatumika kuleta maboresho zaidi katika IGM na taratibu nyingine za kushughulikia malalamiko mgodini.

## Hitimisho

Petra na Williamson Diamonds wamechukua hatua kadhaa muhimu za kujisafisha na tuhuma za zamani. **Wameanza kuweka sawa uhusiano ulioteterekea sana kati ya mgodi na jamii za karibu na mgodi huu**, ambao hapo awali ulisababisha hali ya haki za binadamu kuyumba sana. Hata hivyo, utafiti wa IPIS unaonesha kwamba kuendelea kuboresha uelewa wao na kutatua changamoto na mahitaji ya wakazi wa eneo hilo ndio kutawasaidia Petra na Williamson kutekeleza mipango yao yenye nia njema na kuleta athari chanya.

Hitimisho la ripoti hii linajikita kwenye matokeo tofauti yaliyo kwenye **maeneo sita ya msingi** yanayounda msingi wa kuleta mapendekezo. Haya ni:

(1) Hatua muhimu zinachukuliwa kurejesha na kujenga upya mahusiano na jamii

(2) Maboresho yanaonekana katika kuzuia ukiukwaji wa haki za binadamu, lakini madhara bado yanaripotiwa

(3) Mwanzo mzuri wa kushughulikia malalamiko, lakini kupata sawa fidia baada ya kuumizwa bado ni kazi

(4) Ingawa mahakama inashughulikia mapungufu ya awali na kurejesha kuaminiana, miundo sahihi ya kushirikiana na jamii bado haijawekwa kikamilifu.

(5) Kuna tofauti kubwa kati ya ahadi zilizoko kwenye sera za kampuni kupitia maandishi na uhalisia katika jamii

(6) Madhara kupitia imani iliyoyumba yanafifisha mahusiano chanya ya muda mrefu ya jamii

Kwa mantiki hii, IPIS inaleta **mapendekezo kadhaa maalum** ya kuboresha mahusiano na jamii, kupunguza madhara na kuhakikisha upatikanaji wa dhati wa fidia. Kiujumla, kuishirikisha jamii kwa dhati na kuzingatia vema viwango vya juu vya haki za binadamu na utunzaji wa mazingira kunapaswa kuwa ni juhudi za Petra na Williamson Diamonds, kama wanalenga kutekeleza ahadi zao wakati wa kufanya biashara kutokana na athari jamii ilizopata kutokana na mgodi.

Soma ripoti kamili kwenye: **https://ipisresearch.be/publication/petra-diamonds-attempts-to-come-clean-with-its-tarnished-past-in-tanzania/**

# MAPENDEKEZO

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, IPIS inaweza kupendekeza mapendekezo kadhaa maalum. Pamoja na kwamba mapendekezo haya yanahusu zaidi Petra na Williamson Diamonds, pia yanabeba mambo muhimu kwa wadau wengine muhimu, kama Synergy, wafanyakazi wa IGM na wachunguzi wa kujitegemea, Leigh Day, PwC, na mamlaka za ndani na za kitaifa nchini Tanzania.

Kwa kuongezea, baada ya kujifunza mengi kutokana na utafiti huu kifani ambao unaweza kutumika kwenye hali kama hizo mahali pengine katika sekta ya madini, mapendekezo kadhaa haya pia yanafaa kwa waendeshaji wengine wa kwenye sekta ya madini.

### Kuzuia na kupunguza madhara

1. Boresha zaidi **mipaka ya eneo la uwekezaji la Williamson na kukuza uelewa** juu ya suala hili, kwani mpangilio wa sasa wenye miamba iliyochorwa iliyowekwa nje ya eneo unaendelea kuleta mkanganyiko juu ya suala hili.

2. Hakikisha kwamba wafanyakazi wote pamoja na makandarasi wasiohusika moja kwa moja wa usalama na maafisa wa polisi wa Tanzania wanaojihusisha na operesheni za usalama katika mgodi wa Williamson wanapatiwa mafunzo mara kwa mara na kuheshimu **Miongozo ya Kutii Bila Shuruti Usalama na Haki za Binadamu** na kujiepusha na matumizi ya nguvu isipokuwa pale tu wanajilinda kihalali.

**3. Toa ripoti** kwa umma na kwa kina **matukio yote yanayohusiana na uvamizi**, na taarifa za kina juu ya majeraha, vifo, kuwekwa kizuizini na matumizi ya nguvu, ili kuwezesha ufuatiliaji na uangalizi wa nje.

4. Toa ripoti kwa umma juu ya juhudi zilizofanywa katika kutekeleza Utaratibu wa Petra wa **Kuheshimu Watetezi wa Haki za Binadamu**, hasa kuhusu juhudi za kuepuka kwamba wahanga ni sauti muhimu za wahalifu zilizonyamazishwa katika muktadha mpana wa kisiasa wa ndani.

5. Hakikisha **ufuatiliaji** wa kutosha na wa wazi **wa bwawa la kutunzia makinikia (kwa muda) la mgodi** katika mgodi wa Williamson ili kuhakikisha kuwa ni - na linabaki - kulingana na mahitaji ya uhifadhi salama wa makinikia. Adhere to **international best practice standards on tailings management** and prioritise the implementation of, at minimum, the Global Industry Standard on Tailings Management to maximally prevent, mitigate and monitor actual or potential harm to people and the environment as a result of operations at the Williamson mine.

6. Fuata **viwango vya kimataifa vya taratibu bora za usimamizi wa makinikia** na kuweka kipaumbele utekelezaji wa, kwa kiwango cha chini, Kiwango cha Kimataifa cha Usimamizi wa makinikia viwandani ili kuzuia, kupunguza na kufuatilia madhara halisi au yanayoweza kutokea kwa watu na mazingira kutokana na matokeo ya shughuli katika mgodi wa Williamson.

7. Hakikisha uzingatiaji wa **viwango vya kusimamia haki za binadamu**, kama ilivyoainishwa na Miongozo ya OECD ya Biashara za Kimataifa juu ya Maadili ya Biashara ya Kuwajibika na Kanuni za Uongozi wa Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu, kuzuia, kupunguza na kuhesabu athari zozote mbaya kwa watu na mazingira kama matokeo ya shughuli katika mgodi wa Williamson.

8. Serikali ya Tanzania na taasisi zake husika zitengeneze mazingira kabambe ya udhibiti na uwajibishaji kwenye mwenendo wa biashara na kuongeza uwezo wake wa kufuatilia na kutekeleza kanuni na mahitaji.

### Kuhakikisha upatikanaji sawa wa fidia

1. Tengeneza **miongozo, muundo na taratibu za mipango yote ya kushughulikia malalamiko** zilizowekwa katika mgodi wa Williamson **zipatikane hadharani**, na uhakikishe uhamasishaji endelevu, wa kiutendaji na wenye kulenga mahitaji maalum kwa jamii zilizo karibu.

2. Hakikisha **michakato ya kushughulikia malalamiko ni ya uwazi na ya kutabirika** kwa kutoa taarifa za wakati na za mara kwa mara kwa walalamikaji juu ya hatua tofauti za utaratibu, muda na hali ya kushughulikia malalamiko yao, pamoja na maendeleo ya jumla ya utekelezaji wa utaratibu wa kushughulikia malalamiko.

3. Hakikisha kwamba kushughulikia malalamiko si mchakato wa kuangalia upande mmoja wa kulazimishia lakini badala yake kama mchakato wa **kushirikishana na kuwahusisha walalamikaji** katika hatua zote za mchakato, ikiwa ni pamoja na maamuzi kuhusu uhalali na fidia, na kwa kukomesha matumizi yoyote ya lugha ya kuudhi au ya kutishiana, kufokeana au hatua kutendwa na wanaoshughulikia malalamiko.

4. Hakikisha taratibu zote za kushughulikia malalamiko zinategemea **ujifunzaji endelevu**, sio tu kwa kujumuisha ufuatiliaji huru na ujifunzaji wa somo katika muundo wao, lakini pia kwa kuhakikisha (a) utafutaji na uchakataji wa kutosha wa maoni ya walalamikaji, (b) taarifa ya uwazi juu ya maendeleo na tathmini, na (c) kuzingatia maoni ya uchunguzi na tathmini ya mtu wa tatu.

5. Hakikisha upatikanaji sawa wa fidia kupitia IGM kwa kuhakikisha kwamba walalamikaji wote wanaweza kupata **msaada wa bure na huru wa kisheria** wakati wote wa mchakato mzima wa kushughulikia malalamiko (na sio tu wakati wa taarifa ya uamuzi wao wa mwisho), kama ulivyokiukwa awali na Petra.

6. Hakikisha **IGM inawajibika kwenye masuala ya kijinsia na hatarishi ya walalamikaji** kwa kuhakikisha: (a) upatikanaji wa wataalam wa kujitolea miongoni mwa wafanyakazi wa IGM, (b) mafunzo maalum na endelevu kwa wafanyakazi wote, (c) ujumuishaji wa msaada wa kisaikolojia, kijamii na kitabibu wakati wote wa mchakato, (d) upatikanaji wa msaada huo kwa walalamikaji walio katika mazingira magumu kujiandaa na kuanza kutoa uzoefu kupitia sononа, na (e) chaneli salama na isiyojulikana kwa walalamikaji kutoa dukuduku zao au kuripoti tabia isiyofaa ya wafanyakazi wa IGM.

7. Hakikisha fidia **inaendana na uzoefu na matarajio mbalimbali** ya wale wanaotafuta kugangwa mioyo, kwa kuzingatia sana hali halisi ya kila siku ya watu walioathirika na utofauti wa mahitaji yao, kwa muda mfupi na mrefu.

8. Hakikisha **fidia inalipwa kwa ajili ya hasara na madhara yote yaliyotokana na kuvuja kwa bwawa la la kuchenjulia makinikia Novemba 2022** kwa kuzingatia kwa mapana upotevu kamili, ikiwa ni pamoja na hasara kwa makundi na watu binafsi waliohusika na shughuli zisizo rasmi, kama uchimbaji mdogo wa madini.

9. Hakikisha **ardhi iliyoathiriwa na uvujaji wa bwawa la makinikia Novemba 2022 ambalo liko nje ya eneo la mgodi inarejeshwa vema kwenye hali yake ya awali** ili iweze kutumika tena kwa kilimo na matumizi mengine yote, kama inavyotakiwa, na wakazi wake.

### Kujenga imani ambayo rahisi kupotea na mahusiano mazuri ya kudumu na jamii

1. Hakikisha **ushiriki wa jamii wenye tija** sio shughuli inayojitegemea, lakini inakuwa ni kiini cha juhudi na shughuli zote za kampuni. Hii inahitaji miundo rasmi ya watu kujitolea na fursa za mara kwa mara za ushiriki usio rasmi kwa kuhamasisha wafanyakazi wa kampuni kutoka maeneo yao ya kazi na kuwa na mahusiano na jamii za karibu yao katika muktadha wao wa ndani.

2. Hakikisha kuwa ushiriki wa jamii sio mchakato wa upande mmoja wala wa kipekee, bali unategemea **mazungumzo ya pamoja na mashauriano yenye ufanisi** ya makundi yote kuhusu mambo yanayowahusu. Hii inahitaji uelewa mzuri wa udhaifu, mahitaji na utofauti uliopo kwenye jamii ili kuepuka kuacha nyuma makundi yaliyotengwa au yasiyoweza kupaza sauti sana au kutegemea wadau waliochaguliwa kushirikiana na au kuzungumza kwa niaba ya jamii.

3. Kuhakikisha kuwa **mifugo inayoingia katika eneo la uwekezaji lisilo na uzio inarejeshwa salama kwa mmiliki** wake bila ya kuwekewa faini kubwa wakati huu wa kuirudisha, kama sehemu ya juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa lengo kuu la mgodi ni kuepuka kuhatarisha maisha ya watu zaidi ya inavyotarajiwa.

4. Hakikisha kuna fedha za ziada ili kuepuka kushindwa kuachana na **mradi uliotangazwa wa uchimbaji mdogo wa madini** na kusaidia majaribio yake. Uchimbaji mdogo wa madini ni mustakabali muhimu kwa wakazi wengi wa eneo hilo ambao wameshuhudia mipango mingi kama hiyo ikiondolewa mara kwa mara. Kurudiarudia kuachana na miradi kunasababisha sana hisia za kutelekezwa na kutoaminiana.

5. Hakikisha kwamba kiasi chochote cha makubaliano ya kumaliza mgogoro kilichofikiwa kinaonesha gharama halisi ya maisha kupitia mipango ya ufadhili iliyopangwa kushughulikia migogoro. Pale ambapo kiasi hicho kinakuwa kimepungua, toa fursa ya kuongeza fedha ili kuepuka fidia ya kiwango cha chini kupitia mpango, kuwekeza katika kuleta suluhisho na athari za muda tu, au kuachana na miradi iliyotangazwa kwa sababu gharama zinaonekana kuwa kubwa kuliko zilivyokuwa hapo awali.

Independent research and capacity enhancement for *durable peace, sustainable development and human rights*

IPIS

V.U. Filip Reyniers, Directeur, IPIS vzw, Italiëlei 98A, 2000 Antwerpen I Layout: BRUSK Design I D/2023/4320/18